# HALMASHAURI YA WILAYA YA BUMBULI

## MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI YA BUMBULI TAREHE 26/11/2021.

**A) WAJUMBE WALIOHUDHURIA**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mulsary A. Lukindo | Mwenyekiti |
| 2. | Simon Mwaiteleke | Katibu |
| 3. | Kelvin H. Lefi | Mjumbe |
| 4. | Nelson Masaki | Mjumbe |
| 5. | Glory R. Mushi | Mshauri wa sheria |
| 6. | Denis Kamara | Mshauri wa sheria |

**B) SEKRETARIETI.**

1. Joseph R. Maganga
2. Ally Fakhi

**AJENDA NA. AJENDA NA. 01/BDC/MN/11/2021: KUTEUA MWENYEKITI WA MUDA**

Kabla ya kufungua kikao katibu alitoa taarifa ya udhulu wa mwenyekiti wa Bodi ya zabuni na kutoa muongozo kwa wajumbe ili waweze kuchagua mwenyekiti wa muda, ambapo Nd. Mulsary Lukindo alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa kuendesha kikao hicho.

**Ajenda Na. AJENDA NA. 02/BDC/MN/11/2021: KUFUNGUA KIKAO**

Mweyekiti alifungua kikao mnamo saa 9:47 Alasiri ambapo aliwasihi wajumbe kuwa watulivu na kushiriki kikamilifu katika kikao hicho kwa muda wote wa kikao.

Pia aliwataka wajumbe wachangie hoja zitakazowasilishwa kwa weledi na maslahi ya Halmashauri.

**Ajenda Na. AJENDA NA. 03/BDC/MN/11/2021: KUPITISHA AJENDA**

Katibu aliwasilisha ajenda 13 za kikao hicho na baadaye wajumbe walizipitisha kama ifuatavyo :-

1. Kuteua Mwenyekiti wa muda
2. Kufungua Kikao
3. Kusoma na Kuthibitisha Ajenda
4. Kujadili Mapendekezo ya kuhuisha mkataba wa mtalaamu Mshauri wa jengo la makao makuu ya Wilaya ya Bumbuli katika eneo la Kwehangala.
5. Mapendekezo ya kutumia njia ya **"Force Account"** na kupitisha Mafundi na wauzaji wa vifaa vya ujenzi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.



CamScanner

i. Ujenzi wa madarasa elimu msingi kiasi cha Tshs.**187,110,350.00**
ii. Ujenzi wa Maabara na vyumba vya Madarasa ya Elimu Sekondari Tshs.**337,500,000.00**
iii. Ukamilishaji wa maboma ya Zahanati na ujenzi wa kituo cha Afya Tshs.**650,000,000.00**
iv. Ujenzi wa Nyumba ya Mkururgenzi Mtendaji wa Halmashauri Tshs.**150,000,000.00**
v. Ujenzi wa madarasa 54 na Nyumba ya Mtumishi kwa Fedha UVIKO 19 **Tsh. 1,170,000,000.00**

6. Mengineyo
7. Kufunga kikao

**AJENDA NA. AJENDA NA. 04/BDC/MN/11/2021: KUJADILI MAPENDEKEZO YA KUHUISHA MKATABA WA MTALAAMU MSHAURI WA JENGO LA MAKAO MAKUU YA WILAYA YA BUMBULI KATIKA ENEO LA KWEHANGALA**

Iliwasilishwa taarifa kuhusiana na mapendekezo ya kuhuisha mkataba wa mtaalamu mshauri ambapo mnamo tarehe 25/05/2018 Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli iliingia Mkataba na kampuni tajwa hapo juu kwa ajili ya ushauri na usimamizi wa mradi wa ujenzi wa jengo la Utawala la Halmashauri eneo la Kwehangala kwa gharama ya Tshs **253,664,107.38** sawa na asilimia sita (6) ya thamani ya gharama ya ujenzi ya Tshs **4,227,735,123.00** kwa mujibu wa mkandarasi aliyeshinda zabuni ambaye ni kampuni ya Advent Construction Ltd

Kutokana na shida ya upatikanaji wa fedha mkandarasi aliiomba Halmashauri kusitisha nae mkataba baada ya mwaka mmoja, hata hivyo kipindi chote cha majadiliano na mkandarasi mtaalam mshauri amekuwa akitumika katika kutoa ushauri maelekezo na Halmashauri haijawahi hata kumpa taarifa yoyote kama mkataba unavyoeleza katika masharti ya jumla kipengele cha (65.1) (65.2) (a) mpaka (f) .

Hivyo, taarifa hii imewasilishwa kwenye Bodi ya Zabuni kama chombo chenye maamuzi na ushauri kwa Mkurugenzi kwani hata mkataba wa awali ulikuwa umetunukiwa na Bodi ya zabuni na hata maamuzi ya mwisho yataamriwa na bodi ya zabuni kwa mujibu wa sheria No.7 ya mwaka 2011 na kanuni zake za mwaka 2013 ikisomwa pamoja na marekebisho ya mwaka 2016 kifungu (35) 1-6. Aidha, imeshauriwa kwamba Halmashauri ijiridhishe vya kutosha kwa hatua yoyote itakayochukuliwa juu ya mtaalamu mshauri isije ikaingia kwenye mgogoro na kuigharimu Halmashauri.

Mchanganuo wa malipo yaliyofanyika ni kama ifuatavyo.

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Gharama za mkataba wa awali ni Tshs **253,664,107.38** | Kiasi alicholipwa hadi leo ni Tshs **126,823,053.70** | Kiasi kilichobaki kwa mujibu wa mkataba awali Tshs **126,841,053.68** |

*Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa wajumbe wa bodi wameagiza kuwa; Mkataba wa mtaalamu mshauri uhuishwe ili aweze kuendelea na kazi, Aidha timu ya majadiliano iundwe kutoka katika menejimenti kwa ajili ya kufanya majadiliano na Mkandarasi Mshauri (Y&P ARCHITECT LTD) kwa haraka ambapo kiwango atakacholipwa kiwe ni kiwango ambacho Halmashauri itaweza kukimudu.*



CamScanner

**AJENDA NA. 03/BDC/MN/11/2021: KUJADILI NA KUPITISHA MAPENDEKEZO YA UTEKELEZAJI WA MIRADI KWA KUTUMIA NJIA YA FORCE ACCOUNT KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022.**

*Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa kwa wajumbe wa bodi kuwa; Miradi yenye thamani ya **Tsh. 2,494,610,350** ambayo ni Maabara 3 na Madarasa 10 ya Sekondari Tsh. 337,000,000; Miradi ya Afya Tsh. 650,000,000; Nyumba ya Mkurugenzi Tsh. 150,000,000, Ujenzi madarasa ya Shule za Msingi Tsh. 187,110,350 na Ujenzi wa Madarasa 54 ya Sekondari na nyumba(3in1) ya watumishi wa Idara ya Afya kwa kutumia fedha za UVIKO 19 Tsh. 1,170,000,000 itekelezwe kwa njia ya fource account. Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa ilijadiliwa na wajumbe kuridhia njia hiyo kutumia. Aidha, wajumbe walishauri mhandisi wa ujenzi kufanya ufuatiliaji wa karibu wakati wa utekelezaji wa miradi hiyo kwa kuwa baadhi ya mafundi watakaotumika kutekeleza miradi hii hawana uzoefu wa kutosha hivyo wanahitaji usimamizi wa karibu.*

**AJENDA Na. 12/BDC/MN/11/2021 MENGINEYO**

Kikao hakikuwa na mengineyo.

**AJENDA Na. AJENDA NA. 13/BDC/MN/11/2021 KUFUNGA KIKAO**

Kabla ya kufunga kikao Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa kushiriki kikamilifu katika kikao hicho na kuchangia hoja mbalimbali zenye tija kwa maslahi ya Halmashauri. Baada ya kusema hayo alifunga kikao mnamo saa 10:17 Jioni.

**UMETHIBITISHWA NA;**

**KATIBU WA BODI**

JINA Simon Mwaiteleke

**SAHIHI**.....................

**MWENYEKITI WA BODI**

JINA Muhsaly Lukindo

**SAHIHI**.....................